# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# WIZARA YA MAENDELEO YA MIFUGO NA UVUVI

## Mwongozo wa Masoko ya Mifugo



**Agosti, 2012**

## YALIYOMO

YALIYOMO ........ i
DIBAJI ........ ii
1.0 Utangulizi ........ 1
2.0 Biashara ya Mifugo ........ 3
2.1 Usafirishaji wa mifugo kwenda na kutoka mnadani ........ 3
2.2 Nyaraka zinazohitajika katika kusafirisha mifugo ........ 5
2.3 Kupokea mifugo mnadani ........ 7
2.4 Ukaguzi wa Mifugo ........ 7
2.5 Kupanga madaraja ya mifugo ........ 7
2.6 Uuzaji wa Mifugo katika Minada ........ 10
2.7 Ukusanyaji wa maduhuli ........ 11
2.8 Utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa ........ 11
3.0 Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Minada ya Mifugo ........ 13
3.1 Uanzishaji wa Minada ya Mifugo ........ 13
3.1.1 Eneo la mnada wa awali na upili ........ 13
3.1.2 Minada ya awali ya mifugo ........ 13
3.1.2.1 Mchoro na ujenzi wa mnada wa awali ........ 13
3.1.2.2 Mchoro wa mnada wa ng'ombe, mbuzi na kondoo ........ 14
3.1.2.3 Mchoro wa mnada wa nguruwe ........ 14
3.1.2.4 Mchoro mnada wa kuku uonyeshe sehemu zifuatazo:- ........ 14
3.1.3 Minada ya Upili na Mipakani ........ 15
3.1.3.1 Mchoro na ujenzi wa minada ya upili na mipakani ........ 15
3.1.3.2 Mchoro wa mnada wa ng'ombe, mbuzi na kondoo ........ 15
3.1.3.3 Mchoro wa mnada wa nguruwe ........ 16
3.1.3.4 Mcharo wa mnada wa kuku ........ 16
3.2 Usimamizi na Uendeshaji wa Minada ........ 18
3.2.1 Majukumu ya wafanyakazi katika mnada ........ 18
3.2.1.1 Mkuu wa mnada/ Msimamizi wa minada wa wilaya ........ 18
3.2.1.2 Afisa Mkaguzi wa Afya ya Mifugo ........ 19
3.2.1.3 Mhasibu ........ 19
3.2.1.4 Dalali ........ 19
3.2.1.5 Mpanga madaraja ya mifugo ........ 19
3.2.1.6 Mkuu wa usalama wa raia mnadani ........ 20
3.3 Ratiba ya mnada ........ 20
3.4 Usafi, ukarafati, ukarabati na ulinzi wa minada ........ 20
4.0 Hitimisho ........ 21

## DIBAJI

Usimamizi pamoja na uendeshaji wa masoko na biashara ya mifugo hapa nchini ulikuwa unafanywa na Mamlaka ya Undelezaji wa Mifugo (LIDA) iliyoundwa mwaka 1974 baada ya utaifishaji wa makampuni yaliyomilikiwa na sekta binafsi kwa ajili ya usimamizi wa shughuli zote za mifugo hapa nchini. LIDA ilifanya shughuli hizo chini ya kampuni tanzu ya kusimamia masoko na biashara ya mifugo iliyojulikana kama Kampuni ya Biashara ya Mifugo Tanzania (KABIMITA). Aidha, ilikuwepo kampuni nyingine ya Tanganyika Packers Limited (TPL) ilijishughulisha na usindikaji na biashara ya nyama na mazao yake. Katika kipindi hicho bei ya mifugo ilitolewa kulingana na ubora wake na pia biashara iliendeshwa kwa uwazi kwa njia ya kunadisha mifugo. Vile vile matumizi sahihi ya miundombinu ya minada ilizingatiwa kama vile matumizi ya mizani na kiringe cha kunadia.


Kutokana na mabadiliko ya kiuchumi duniani mwishoni mwa miaka ya 1980 Tanzania ililazimika kufuata sera za uchumi wa soko, ambapo shughuli zote za biashara ikiwemo biashara ya mifugo ziliachwa kufanywa na Sekta Binafsi. Mara baada ya mabadiliko haya ya sera uendeshaji wa biashara na usimamizi wa masoko ya mifugo ulianza kulegalega, ambapo biashara ikawa inafanywa bila kuzingatia misingi stahili kama vile kuzingatia ubora wa mifugo, kunadisha na kutotumia uzito kama kigezo cha bei. Hii ilifanya biashara kuwa ya mapatano, kutozingatia ubora na uzito kupimwa kwa kukadiria, ambapo wafugaji ndio wamekuwa wahanga wa hali hii. Mambo haya yaliwavunja moyo wafugaji kuzalisha mifugo kwa kuzingatia ubora. Aidha, mifugo inayozalishwa kwa kiwango kikubwa imeshindwa kuzalisha nyama yenye ubora na kushindwa kufikia masoko maalum yenye bei nzuri ya ndani na nje ya nchi.

Ili kuweza kuunda upya tasnia ya nyama ikiwemo biashara ya mifugo hai pamoja na nyama serikali ilianzisha Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na kanuni zake za mwaka 2011. Utekelezaji wa sheria hii unafanywa kwa njia mbalimbali ikiwemo kuandaa miongozo ya kuelemisha wadau wa tasnia, ambapo Wizara imeandaa mwongozo wa masoko ya mifugo. Mwongozo huu unasisitiza mambo muhimu ya kuzingatia katika masoko na biashara ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuwa na miundombinu sahihi, taratibu za biashara ya mifugo, ubora wa mifugo na mfumo wa kupanga bei kwa njia ya ushindani. Hii inalenga kuhamasisha uzalishaji wa mifugo bora, kuongeza pato la mfugaji mmoja mmoja na la Taifa kwa ujumla.

Mwongozo huu pia, unahamasisha mamlaka zinazohusika na kuanzisha, kusimamia na kuendesha minada ya mifugo kuzingatia vigezo sahihi ili kuboresha mfumo mzima wa biashara ya mifugo hapa nchini. Vile vile mwogozo umeweka bayana majukumu ya kila mdau wa masoko ya mifugo ambapo atalazimika kuyatimiza. Aidha, lengo la mwongozo huu ni kusaidia kutoa elimu pale ambapo

inahitajika kwa ajili ya kuongeza ufanisi katika masoko (*marketing efficience)* na kuboresha ukusanyaji wa maduhuli ya serikali katika kuongeza pato la Taifa.

Ni matumaini ya Wizara yangu kuwa kila mdau atatekeleza majukumu yake kama yalivyoelezwa kwenye mwongozo huu katika kuchangia na kuboresha mfumo mzima wa uendeshaji wa biashara ya mifugo hapa nchini na kukidhi viwango vya masoko ya mifugo vya kitaifa na kimataifa.



Dr. David Mathayo David (MB)
**Waziri wa Maendeleo a Mifugo na Uvuvi**

**Dar Es Salaam**
**Juni, 2012**

## SEHEMU YA I

## 1.0 Utangulizi

Tanzania ina rasilimali kubwa ya mifugo takribani ng'ombe milioni 21.3, mbuzi milioni 15.2, kondoo milioni 6.4, nguruwe milioni 1.9 na kuku milioni 58 (NBS, 2011), ambayo ikiendelezwa kibiashara itatoa mchango mkubwa katika kipato cha mfugaji mmoja mmoja na uchumi wa nchi kwa ujumla. Kwa sehemu kubwa mifugo hii hufugwa kwa sababu za kijamii zaidi, sehemu ndogo tu ndiyo ambayo huingia kwenye biashara. Biashara ya mifugo katika maeneo mengi hapa nchini haizingatii ubora wa mifugo (madaraja) na bei hupangwa kwa msingi wa mapatano hivyo kutokuwa wazi. Hii ni kwa sababu wafugaji wengi huuza mifugo pale ambapo kuna mahitaji ya fedha na sio kwa kuzingatia vigezo vya ubora wa mifugo. Aidha, mahitaji ya soko la ndani hayashawishi wafugaji kuzalisha na kuuza mifugo yenye ubora (madaraja) wa viwango vya kimataifa na hivyo kuchangia kiasi kidogo katika pato la mfugaji mmoja mmoja na taifa kwa ujumla. Kwa mfano, mwaka 2011/2012 takwimu zinaonyesha takribani ng'ombe **1,015,067** mbuzi **771,967** na kondoo **179,289** wenye thamani ya shilingi **bilioni 775.4** waliuzwa kwenye minada mbalimbali hapa nchini na ng'ombe **3,362** na mbuzi/kondoo **4,060** wenye thamani ya shilingi **bilioni 3.81** waliuzwa nje ya nchi, hususan Comoro. Aidha, tani **31.6** za nyama ya ng'ombe, tani **647** za nyama ya mbuzi na tani **151.8** za nyama ya kondoo zenye thamani ya shilingi **bilioni 19.3** ziliuzwa katika nchi za Oman na Kuwait.

Aidha, biashara ya mifugo hapa nchini imekuwa ikiendeshwa bila kuzingatia taratibu zilizopo kwa mujibu wa Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003, Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008, Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008, Sheria ya, Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji wa Mifugo Na. 12 ya mwaka 2010, pamoja na kanuni zilizoandaliwa chini ya sheria hizi. Hali hii imeleta athari nyingi za kibiashara ikiwemo ueneaji wa magonjwa, wizi wa mifugo, uharibifu wa mazingira, matumizi yasiyoridhisha ya miundombinu ya masoko, usimamizi mdogo katika kutunza na uendelezaji wa miundombinu ya masoko na biashara ya magendo ya mifugo mipakani ambapo inakadiriwa kuwa zaidi ya ng'ombe **300,000** huvuka mipaka na kuuzwa nje ya nchi kila mwaka.

Hapa nchini biashara ya mifugo hufanyika katika minada ambayo ni miundombinu muhimu katika kufanikisha biashara hii na ni kiungo kati ya wafugaji na wafanyabiashara ambayo huanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo ya mwaka 2011 kifungu cha 4 sehemu ya 1 na 2. Kuna aina tatu za minada ambayo ni minada ya awali, upili na mipakani. Minada ya awali ya mifugo hupatikana katika maeneo ya ufugaji (vijijini), kwa kawaida minada hii ni midogo yenye

uwezo wa kupokea ng'ombe hadi kufikia **400** kwa siku ya mnada. Minada ya awali husimamiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Minada ya upili ya mifugo hupatikana katika maeneo yenye makutano ya njia za mifugo kutoka kwenye minada ya awali au maeneo yenye walaji wengi, kwa kawaida minada hii ina uwezo wa kupokea ng'ombe zaidi ya **400** kwa siku ya mnada na husimamiwa na Serikali Kuu. Minada ya mipakani hupatikana katika maeneo ya mipaka ya nchi ili kuwezesha kufanyika kwa biashara halali ya mifugo na nchi jirani. Kwa kawaida minada hupokea mifugo kutoka minada ya awali na ile ya upili na husimamiwa na Serikali Kuu.

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuongeza ufanisi katika usimamizi, uratibu wa biashara ya mifugo na uendelezaji wa miundombinu ya masoko. Mwongozo huu unalenga kuelekeza wadau wakiwemo wafugaji, wafanyabishara, wasimamizi, waratibu na wadau wengine wa biashara ya mifugo kuhusu mbinu na taratibu za kuzingatiwa katika biashara ya mifugo. Aidha, mwongozo unatoa tafsiri na maelekezo ya vigezo na namna ya kuanzisha, kutunza, kuendeleza na kusimamia miundombinu ya masoko ya mifugo na masuala mengine muhimu ili kufanikisha shughuli za masoko na biashara ya mifugo hapa nchini.

## SEHEMU YA II

### 2.0 Biashara ya Mifugo

Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2007 na Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 pamoja na Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo za mwaka 2010 zinaelekeza kuwa biashara ya mifugo hai kati ya wafugaji na wafanyabiashara wenye leseni au kati ya wafanyabiashara wenye leseni ifanyike katika sehemu zifuatazo:-

i) Minada ya awali,
ii) Minada ya upili,
iii) Minada ya mipakani,
iv) Machinjio zinazofanya biashara ya kusindika nyama, na
v) Mashamba ya unenepeshaji (feedlot) na ranchi.

Aidha, Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 pamoja na Kanuni ya kupanga madaraja ya mifugo na nyama "The Meat Industry (Livestock and Carcass Grading) regulations", 2010 kifungu Na. 6. inaelekeza kuwa mifugo inayopelekwa minadani, kuuzwa kwa ajili ya kuchinjwa na kuzalisha nyama hususan ng'ombe, mbuzi na kondoo iwe na sifa za ubora wa daraja la Tanzania Bora, Daraja la Kwanza, Daraja la Pili na Daraja la Tatu. Wafugaji wanashauriwa kuvuna mifugo yao kwa kuzingatia umri (ng'ombe miaka 3 – 4, mbuzi na kondoo miaka 1.5 – 2, nguruwe miezi 7 – 12, Kuku wa kienyeji miezi 6 – 9 na kuku wanyama wiki 6 -7) na bila kuathiri vigezo vingine, Aidha, mifugo ya daraja la Nne itumike kwa ajili ya kunenepesha.

### 2.1 Usafirishaji wa mifugo kwenda na kutoka mnadani

Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na kanuni zake za mwaka 2007 za kusimamia usafirishaji wa mifugo kifungu Na. 4 hadi 7, Sheria ya Biashara ya Ngozi Na. 18 ya mwaka 2008 chini ya kanuni ya kuzuia uharibifu wa ngozi kifungu Na. 4 (5 na 6) na Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008 kanuni ya usafirishaji wa mifugo ya mwaka 2010 kifungu Na 8-17, zinaelekeza kuwa usafirishaji wa mifugo kwenda na kutoka minadani uzingatie ustawi wa wanyama, uepuke usambazaji wa magonjwa, uharibifu wa ngozi, upotevu wa uzito na uharibifu wa mazingira. Aidha, inasisitizwa kuwa kupakia na kushusha mifugo kufanyike kwenye maeneo maalum yaliyojengwa kwa ajili ya kazi hiyo. Aidha, msafirishaji wa mifugo kutoka shambani kwenda kwenye minada ya awali au kutoka kwenye minada ya awali kwenda kwenye minada ya upili na mipakani, machinjioni au vituo vya kupumzishia mifugo azingatie mambo yafuatayo:-

(a) Mifugo ikaguliwe na kuhakikishwa kuwa haina ugonjwa wowote wa kuambukiza,
(b) Kuwa na kibali cha kusafirisha mifugo kwenda mkoa mwingine ambacho kitaishia kwenye mnada wa upili, mpakani, machinjio au kituo cha

kupumzishia mifugo kinachotolewa na Bwana Mifugo mwenye dhamana; endapo mifugo hiyo haitanunuliwa, kibali kingine cha kusafirishia mifugo kuirudisha ilikotoka kitahitajika,

(c) Kutopeleka mnadani mifugo iliyotibiwa kwa dawa ya kiuavijasumu (antibiotics) hadi muda salama ulioelekezwa katika maelezo ya dawa utakapotimia,

(d) Kupeleka mnadani mifugo iliyochaguliwa kwa ajili ya kuuza ili kuzuia maambukizi ya magonjwa kwa mifugo inayosindikiza,

(e) Kusafirisha mifugo kutoka kwenye boma kwenda kwenye mnada umbali usiozidi kilometa 30 kwa kuswaga,

(f) Kusafirisha mifugo iliyonunuliwa kwenda kwenye mnada wa upili, mpakani au kituo cha kupumzishia mifugo kabla ya kupelekwa machinjioni kwa kutumia malori,

(g) Kusafirisha nguruwe kutoka shambani kwenda mnadani kwa kutumia lori, *pick up* au mkokoteni unaovutwa na wanyama kazi,

(h) Kusafirisha kuku kwenye tenga au kreti kwa kutumia usafiri wowote kutoka shambani kwenda sokoni au kutoka soko moja hadi jingine au kwenda machinjioni,

(i) Kusafirisha mifugo kwa kuzingatia Sheria ya Ustawi wa Wanyama Na. 19 ya mwaka 2008, kanuni ya usafirishaji wa wanyama ya mwaka 2010 kifungu Na. 8 hadi 16 inaelekeza kuwasafirisha wanyama kiutu ikiwa ni pamoja na kuwapunguzia mateso yanayotokana na kukosa huduma muhimu (maji, malisho, n.k.) na nafasi ya kutosha (kukanyagana, kukosa hewa) kama inayoelekezwa katika Jedwali 1, 2 na 3 kulingana na mahitaji ya aina ya mfugo,

(j) Kupumzisha mifugo inayosafirishwa kwa kutumia malori baada ya umbali wa kilometa 300 ili wanywe maji na kupata malisho katika vituo vilivyotengwa na Serikali.

**Jedwali 1: Mahitaji ya nafasi wakati wa kusafirisha ng'ombe kwa malori au gari moshi**

| **Aina** | **Wastani wa Uzito (kilo)** | **Eneo kwa mita za mraba kwa ng'ombe mmoja** |
|---|---|---|
| Ndama wadogo | 55 | 0.30-0.40 |
| Ndama wa kati | 110 | 0.40-0.70 |
| Ndama wakubwa | 200 | 0.70-0.95 |
| Ng'ombe wa ukubwa wa kati | 550 | 1.30-1.60 |

**Jedwali 2: Mahitaji ya nafasi wakati wa kusafirisha mbuzi na kondoo kwa lori au gari moshi**

| **Aina** | **Wastani wa Uzito (kilo)** | **Eneo kwa mita za mraba kwa kondoo/mbuzi mmoja** |
|---|---|---|
| Kondoo mdogo | Zaidi ya 26 | 0.2 |
| Kondoo mkubwa | Chini ya 55 | 0.2-0.30 |
| | Zaidi ya 55 | Zaidi ya 0.30 |
| Mbuzi | Chini ya 35 | 0.20-0.30 |
| | Kati ya 35 hadi 55 | 0.30-0.40 |
| | Zaidi ya 55 | 0.40-0.75 |

**Jedwali 3: Mahitaji ya nafasi wakati wa kusafirisha nguruwe kwa malori au gari moshi**

| **Aina** | **Eneo kwa mita za mraba kwa nguruwe mmoja** |
|---|---|
| Vitoto vya nguruwe vyenye umri wa wiki 8 | 0.1 |
| Chini ya kilo 20 | 0.2 |
| Kati ya kilo 20 hadi 50 | 0.3 – 0.4 |
| Zaidi ya kilo 50 | 0.4 – 0.7 |

**Jedwali 4: Mahitaji ya nafasi wakati wa kusafirisha kuku kwa malori au gari moshi**

| **Aina** | **Eneo** |
|---|---|
| Kifaranga cha siku moja | Vifaranga 455 kwa mita moja ya mraba |
| Chini ya kilo 1.6 | 180-200 sentimita za mraba kwa kilo |
| Kati ya kilo 1.6 hadi 3 | 160 sentimita za mraba kwa kilo |
| Kati ya kilo 3 hadi 5 | 115 sentimita za mraba kwa kilo |

## 2.2 Nyaraka zinazohitajika katika kusafirisha mifugo

Kusafirisha mifugo kutoka sehemu moja hadi nyingine kunaweza kutoa mwanya wa wizi wa mifugo na kueneza magonjwa ya mifugo. Ili kuzuia wizi na kudhibiti maambukizi ya magonjwa ya mifugo Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na Kanuni zake za kusimamia usafirishaji wa mifugo kifungu Na. 4 hadi 7 na Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na Kanuni ya Uendeshaji wa masoko ya mifugo ya mwaka 2011 kifungu Na.4 hadi 10 zinaelekeza kuwa mfugaji au mfanyabiashara kuhakikisha anapata nyaraka muhimu za kusafirishia mifugo ambazo ni:-

**Kusafirisha mifugo kutoka kwa mfugaji/shambani kwenda mnadani**

(i) Uthibitisho/kibali wa/cha uhalali wa umiliki wa mfugo unaopelekwa mnadani, unaotolewa na Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa/Kata,
(ii) Uthibitisho/kibali wa/cha hali ya kiafya (magonjwa, mimba) ya mfugo anayesafirishwa ambao unatolewa na Afisa Mifugo mwenye dhamana katika eneo aliko mfugaji/shambani.

**(a) Kusafirisha mifugo kutoka mnadani**

(i) Kibali cha kusafirisha mifugo (livestock movement permit) kutoka mnadani kwenda shambani au kwenda kwenye mnada mwingine au kwenye kituo cha kupumzishia mifugo au machinjioni ambacho kinatolewa na Ofisi ya Ukaguzi wa Afya ya Mifugo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika au Afisa Mkaguzi wa Afya ya Mifugo aliyeteuliwa na Wizara yenye dhamana ya mifugo. Kibali hiki kitatolewa kwa malipo ya kiwango kilichowekwa na wizara yenye dhamana ya mifugo.
(ii) Uthibitisho/kibali wa/cha uhalali wa umiliki wa mfugo unaopelekwa mnadani, unaotolewa na Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji/ Mtaa/Kata au Msimamizi Mkuu wa mnada/Msimamizi wa mnada wa wilaya baada ya kubadilishana taarifa za mifugo iliyouzwa.

**(b) Kusafirisha mifugo nje ya nchi**

(i) Uthibitisho wa uhalali wa umiliki wa mifugo inayosafirishwa,
(ii) Uthibitisho wa afya ya mifugo inayotarajiwa kusafirishwa kinachotolewa na Afisa Mkaguzi wa Afya ya Mifugo anayesimamia eneo la kudhibiti magonjwa ya mifugo (quarantine station),
(iii) Barua ya udhamini wa benki (Letter of credit) inayothibitisha kuwa mifugo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi, inauzwa kupitia taratibu za kibenki,
(iv) Kibali kinachomruhusu kuingiza mifugo kwenye nchi anakopeleka mifugo hiyo,
(v) Kibali cha kusafirisha mifugo nje ya nchi ambacho atakipata kutoka ofisi ya Mkurugenzi wa Huduma za mifugo

**(c) Kibali cha kuingiza mifugo ndani ya nchi**

(i) Kibali cha kuingiza mifugo ndani ya nchi kinachotolewa na Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo nchini,
(ii) Cheti cha kuthibitisha hali ya kiafya ya mifugo kutoka kwenye mamlaka ya huduma za mifugo ya nchi inakotoka mifugo,
(iii) Hati ya malipo ya gharama za kibali cha kuingizia mifugo nchini kama atakavyoelekezwa na Wizara yenye dhamana na mifugo,
(iv) Uthibitisho wa uhalali wa biashara ya mifugo toka nje ya nchi.

### 2.3 Kupokea mifugo mnadani

Upokeaji mifugo mnadani utafanywa na mkuu wa mnada/msimamizi wa minada wa wilaya, mkaguzi wa afya ya mifugo na mkuu wa usalama wa raia ili kuhakikisha kuwa mifugo halali na yenye afya nzuri ndiyo inayopokelewa mnadani. Timu hiyo ihakikishe kuwa:-

(a) Mifugo inayofikishwa mnadani kwa malori au garimoshi inashushwa kwa kutumia miundombinu maalamu ya kushushia mifugo,
(b) Kukusanya na kukagua vibali vya kusafirishia mifugo inayoletwa mnadani.
(c) Kukagua afya ya mifugo inayoletwa mnadani

### 2.4 Ukaguzi wa Afya ya Mifugo Minadani

Mifugo inayopelekwa mnadani hutoka katika maeneo mbalimbali na yenye umbali tofauti, hivyo kuwa na uwezekano wa kujeruhiwa na kuugua wakati wa usafirishaji. Hali hii inalazimu mifugo kuchunguzwa mara ifikapo minadani na endapo itakuwa na dalili za ugonjwa au kujeruhiwa, hatua zifuatazo zichukuliwe:-

(a) Mifugo itengwe na kuwekwa katika zizi/banda la mifugo chini ya uangalizi wa kitabibu.
(b) Sampuli zichukuliwe na zipelekwe kituo cha uchunguzi wa magonjwa ya mifugo kilicho karibu,
(c) Mifugo iliyochini ya uangalizi inaweza kuchinjwa kwa dharura kwa kibali maalum.
(d) Mifugo iliyojeruhiwa kwa kiasi ambacho hataweza kuendelea kuishi wakati wa usafirishaji ichinjwe kwenye karo la dharura lililopo mnadani
(e) Mifugo iliyokufa ifanyiwe uchunguzi (poste-mortem) ili kugundua chanzo cha kifo, na
(f) Mizoga ichomwe katika tanuru (incinerator) la moto au izikwe au itupiwe kwenye shimo maalum la kutupia mizoga (condemnation pit).



### 2.5 Kupanga madaraja ya mifugo

Kutokana na mapungufu yaliyopo katika biashara ya mifugo ya uholela na kutokuwa na uwazi, serikali chini ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 na Kanuni za Upangaji wa Madaraja ya Mifugo na Nyama za mwaka 2011 kifungu 11 (4), imeandaa utaratibu wa kupanga madaraja ya ng'ombe wa biashara ambao ni kipimo cha uwiano kati ya ubora wa mifugo na bei yake. Upangaji madaraja unafanywa kwa kuzingatia uzito, umri na mwonekano wa mifugo. Hivyo, mifugo ifikapo mnadani ipangwe kwenye madaraja yanayotumika nchini ambayo ni Tanzania Bora, la Kwanza, la Pili, la Tatu na la Nne ambayo sifa zake ni kama zilivyoainishwa hapa:-

**Tanzania Bora**

i) Umbo kubwa na misuli minene sana,
ii) Misuli iliyojaa vizuri kuanzia miguu ya nyuma mbavuni mgongoni hadi shingoni,
iii) Umbo pana kwenye kiuno na tako,
iv) Misuli iliyojazia kwenye miguu yote na mapaja,
v) Ngozi nyororo inayomeremeta,
vi) Uzito mkubwa ikilinganishwa na umri
vii) Kama hawajapevuka wanaonekana wana afya nzuri na kuonekana kuwa watafikia uzito mkubwa watakapokomaa.


Picha ya ng'ombe daraja la Tanzania Bora

**a) Daraja la Kwanza**

i) Misuli minene kiasi iliyokaa sawa na imekamilika,
ii) Misuli minene kiasi katika mapaja na miguu ya nyuma,
iii) Umbo pana kiasi, na
iv) Wale ambao bado hawajapevuka wanaonyesha mifupa mikubwa na misuli minene kiasi cha kuonyesha kuwa wakipevuka watakuwa Tanzania Bora.

Picha ya ng'ombe Daraja la Kwanza

**Daraja la Pili**

i) Mnene kidogo kwenye mabega hadi kufikia miguu ya nyuma,
ii) Mpana na mnene kidogo kwenye kiuno na mapaja,
iii) Miguu ya nyuma ni myembamba kidogo,
iv) Wamesinyaa kidogo,
v) Wale ambao bado hawajapevuka, misuli yake ni dhaifu kidogo na myembamba, na
vi) Ng'ombe wa asili wengi wako kwenye kundi hili

Picha ya ng'ombe Daraja la Pili




**b) Daraja la Tatu**

i) Wembamba kiasi kuanzia kwenye mabega hadi miguu
ii) Wana misuli miembamba mwili wote na nyama kidogo
iii) Wanene kwenye umbo kuliko mapaja na miguu
iv) Wamekonda na kuonekana dhaifu
v) Wale ambao hawajapevuka wana ngozi dhaifu
vi) Hawa ni wale waliokosa malisho na waliozaliana kiukoo.

Picha ya ng'ombe Daraja la Tatu




**c) Daraja la Nne**

i) Kiwango cha chini kabisa cha ng'ombe wanaozalishwa Tanzania,
ii) Wamekonda na mifupa inaonekana mwili mzima,
iii) Wembamba nyuma kuliko mbele,
iv) Ni wadhaifu na hawawezi kuswagwa kwa muda mrefu, wengi wanafia njiani kama wakilazimishwa kuswaga kwa masafa marefu,
v) Waliokosa maji na malisho kwa ajili ya ukame, na

vi) Wale ambao hawajapevuka wanaonekana dhaifu na hawawezi kukua na kuzalisha nyama nzuri.

Picha ya ng'ombe Daraja la Nne




## 2.6 Uuzaji wa Mifugo katika Minada

Ili uuzaji wa mifugo uwe uwazi na wa ushindani, utaratibu wa kunadi utumike kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) Mfugaji/mfanyabiashara atoe taarifa ya jinsi, umri, uzito, aina ya mfugo, vyakula na matibabu ya mfugo na matumizi (uzalishaji, unenepeshaji au kuchinja) kwa mpanga madaraja,
(b) Mpanga madaraja apange madaraja ya mifugo baada ya kupokea taarifa za mifugo
(c) Mpanga madaraja atoe taarifa za idadi, jinsia, daraja, umri, uzito, matumizi ya mifugo (uzalishaji, unenepeshaji au kuchinja) kwa Dalali,
(d) Dalali afungue shughuli za mnada kwa kutoa ishara ya kuanza kwa kugonga kengele au kupiga filimbi,
(e) Uuzaji wa mifugo minadani ufanyike katika kiringe cha kunadi chini ya usimamizi wa dalali,
(f) Dalali anadi mifugo kwa kuzingatia kipengele (c) hapo juu, mnunuzi atakayetamka bei ya juu ndiye atakayeuziwa mfugo baada ya muuzaji kuafiki bei,
(g) Dalali anadi mfugo mmoja mmoja au kundi ilimradi liwe na ubora wa aina moja,
(h) Dalali ahakikishe kuwa muuzaji analipwa malipo yake halali ya mauzo na mnunuzi anapatiwa nyaraka za mifugo hiyo baada ya kulipa ushuru wa soko na kibali cha kusafirishia mifugo,
(i) Dalali afunge mnada baada ya kunadi mifugo yote,
(j) Dalali aandae taarifa ya shughuli za mnada za siku husika ikiwa ni pamoja na idadi, bei, madaraja, uzito na kuwasilisha kwa mkuu wa mnada, na
(k) Mifugo ambayo haikununuliwa irejeshwe kwa wamiliki wao au kuwekwa katika eneo la kupumzishia mifugo wakati wakisubiri siku nyingine ya mnada.

## 2.7 Ukusanyaji wa maduhuli

Biashara ya mifugo inahusisha ukusanyaji wa maduhuli ya serikali ambayo ni ushuru wa soko (*Market fee)* na vibali vya kusafirishia mifugo (*Livestock Movement permit)* kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, na kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo kifungu Na. 13 (1 hadi 4). Ukusanyaji wa maduhuli hayo ufuate Sheria ya Fedha Na. 6 ya Mwaka 2001 (2004) na Kanuni za Fedha za mwaka 2001 ikiwa ni pamoja na utaratibu ulioelekezwa hapa chini:-

(a) Mhasibu wa mnada akusanye na kuwasilisha maduhuli katika mamlaka husika kama inavyoelekezwa katika Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya mwaka 2003 na Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 pamoja na Kanuni za Masoko ya Mifugo za mwaka 2010, kwa kutumia nyaraka za serikali za kukusanyia maduhuli zifuatazo:-
   - i) Stakabadhi ya kupokelea fedha (ERVs),
   - ii) Stakabadhi maalum (Fixed receipts), na
   - iii) Hati ya kuwasilisha malipo benki,

na kuweka kumbukumbu katika Kitabu cha kuingiza fedha taslimu (RCCB),

(b) Kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, na Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo kifungu Na. 13 (3 na 4) inaelekeza kuwa:-
   - i. Ushuru wa soko na wa vibali vya kusafirisha mifugo utakaokusanywa toka minada ya upili na mipakani upelekwe Serikali Kuu, na,
   - ii. Ushuru wa soko toka minada ya awali utabaki katika Mamlaka za Serikali za Mitaa husika. Aidha, ushuru wa vibali vya kusafirisha mifugo katika minada ya awali uwasilishwe Serikali Kuu mara baada ya kukusanywa.

## 2.8 Utunzaji wa kumbukumbu na utoaji wa taarifa

Sheria ya Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji Na. 12 ya mwaka 2010 chini ya kanuni za Utambuzi, Usajili na Ufuatiliaji kanuni za mwaka 2011 kifungu 15 (1 e) na kifungu 33 (1 na 2) inaelekeza kuwa taarifa/kumbukumbu za shughuli za mnada zirekodiwe na kutunzwa. Taarifa hizo zitatolewa kwa mamlaka au taasisi husika ili zitumike katika mipango ya maendeleo. Kumbukumbu muhimu zinazohusu biashara ya mifugo minadani ni pamoja na;

(a) Taarifa za utambuzi, kwa mfano kibali cha kusafirishia mifugo (sehemu ilikotolewa mifugo), aina, cheti cha afya, umri, jinsia, namba ya usajili wa shamba/ranchi, alama ya utambuzi ya mifugo, n.k.
(b) Taarifa za masoko, ikiwa ni pamoja na;tarehe ya mauzo, jumla ya mifugo iliyofikishwa na kuuzwa minadani, uzito wa mifugo, daraja, bei ya mifugo, jina la mfanyabiashara (muuzaji/mnunuzi), jina na namba ya leseni ya dalali, (Jedwali Na. 1),
(c) Taarifa za ukusanyaji maduhuli,
(d) Taarifa za mifugo iliyonunuliwa na ambayo haijanunuliwa na bado ipo kwenye eneo la mnada.

## Jedwali 1: Taarifa za Masoko

| Wilaya | Mnada | Aina ya mifugo | Ng'ombe waliofika mnadani | Idadi ya ng'ombe waliouza na kuruhusiwa kusafirishwa. | | | Wastani wa uzito | Daraja la walio wengi | Wastani wa Bei | Maduhuli yaliyo kusanywa |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | Ndani ya wilaya | Nje ya wilaya | Nje ya mkoa | | | | |
| | | Maksai | | | | | | | | |
| | | Madume | | | | | | | | |
| | | Majike | | | | | | | | |
| | | Mitamba | | | | | | | | |

## SEHEMU YA III

## 3.0 Uanzishaji, Uendeshaji na Usimamizi wa Minada ya Mifugo

### 3.1 Uanzishaji wa Minada ya Mifugo

Minada ya awali, upili na mipakani itaanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Nyama Na. 10 (2006) kifungu 34 sehemu (e) chini ya Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo ya Mwaka 2011 kifungu Na 6 (1 hadi 3) na Na. 7 (1 na 2). Aidha, uanzishaji wa mnada utazingatia sheria nyingine husika ikiwemo Sheria ya Magonjwa ya Wanyama Na. 17 ya 2003, Kanuni ya Kusimamia Usafirishaji wa Mifugo kifungu Na. 17 na 18. Pamoja na sheria hizi, minada ianzishwe kwa kuzingatia vigezo mbalimbali vikiwemo idadi ya mifugo ya biashara ambayo uwepo wa mifugo isiyopungua **25,000** katika mzingo wa kilomita **30** na uwepo wa fursa za biashara hiyo.

#### 3.1.1 Eneo la mnada wa awali na upili

Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 chini ya Kanuni ya Masoko ya Mifugo kifungu Na. 5 (1-3) inaelekeza kuwa eneo linalofaa kwa ujenzi wa mnada wa awali linatakiwa kuwa na sifa zifuatazo:

(a) liwe katika mpango wa matumizi bora ya ardhi yaliyoainishwa na mamlaka husika,
(b) liwe umbali usiopungua kilomita mbili (2) kutoka vyanzo vya maji, mashamba, makazi ya watu, taasisi (mfano shule, zahanati), viwanda na migodi.
(c) liwe kwenye mwinuko usiozidi asilimia 2 na lisilotuamisha maji
(d) lifikike kwa urahisi kwa kutumia njia za mifugo, barabara, reli, anga au majini.
(e) liwe na ukubwa usiopungua **hekta 10** kwa mnada wa ng'ombe/mbuzi/kondoo; **hekta 3** kwa nguruwe na hekta 1 kwa kuku.
(f) Liwe na eneo la huduma muhimu za jamii (mfano sehemu za kuuzia vyakula, vyoo, maji) ambalo haliruhusiwi kujenga makazi ya kudumu.

#### 3.1.2 Minada ya awali ya mifugo

Pendekezo la kuanzisha minada ya awali litatolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya mifugo, akiridhia minada itaanzishwa kama ilivyoelezwa kwenye Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo kifungu Na. 4 (1). Minada hii itajengwa, itasimamiwa na itaendeshwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kuzingatia mambo yafuatayo:-

##### 3.1.2.1 Mchoro na ujenzi wa mnada wa awali

Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006 chini ya Kanuni ya Masoko ya Mifugo kifungu Na. 6 na 7 (1 na 2) inaelekeza kuwa minada ijengwe kwa kufuata

michoro iliyohakikiwa ili kuweka viwango vya ubora vilivyokubalika na kuwa na mfumo mmoja wa ujenzi wa minada hapa nchini. Ili kuwa na mfumo huo utaratibu ufuatao uzingatiwe:-

(a) Mchoro wa mnada wa mifugo uandaliwe na kupitishwa na Wizara yenye dhamana ya mifugo,

(b) Ujenzi wa mnada uzingatie Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005.

#### 3.1.2.2 Mchoro wa mnada wa ng'ombe, mbuzi na kondoo

Ujenzi wa mnada ya mifugo uzingatie matakwa ya Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo kifungu Na. 5 (1-3) kama ilivyoonyeshwa kwenye kiambatanisho Na. 1 ambacho kinaonyesha sehemu zifuatazo:-

i) Sehemu ya kushusha na kupakia mifugo,
ii) Mazizi ya mifugo inayouzwa, iliyonunuliwa na mifugo iliyotengwa kwa sababu mbali mbali,
iii) Mizani, kibanio, kiringe cha kunadi mifugo na majukwaa ya wauzaji na wanunuzi.
iv) Mabirika ya maji na eneo la malisho,
v) Tanuru/shimo la kuteketeza/kuzika mizoga na taka nyingine,
vi) Ofisi, nyumba ya mlinzi na vyoo vinavyokidhi mahitaji
vii) Sehemu ya kuchinjia kwa dharura (emergency slaughter slab)
viii) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada,

#### 3.1.2.3 Mchoro wa mnada wa nguruwe

i) Sehemu ya kushusha na kupakia nguruwe,
ii) Mazizi yenye paa kwa ajili ya nguruwe wanaouzwa, walionunuliwa na waliotengwa kwa sababu mbali mbali,
iii) Mizani, kibanio, kiringe cha kunadi Nguruwe na majukwaa ya wauzaji na wanunuzi.
iv) Mabirika ya maji na eneo la kulishia ndani ya mazizi,
v) Tanuru/shimo la kuteketeza/kuzika mizoga na taka nyingine,
vi) Ofisi, nyumba ya mlinzi na vyoo vinavyokidhi mahitaji,
vii) sehemu ya kuchinjia kwa dharura (emergency slaughter slab)
viii) Jiko la kuchemshia maji
ix) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada

#### 3.1.2.4 Mchoro mnada wa kuku uonyeshe sehemu zifuatazo:-

i) Mazizi yenye paa kwa ajili ya kuku wanaouzwa, walionunuliwa, waliotengwa kwa sababu mbali mbali, yaliyo simikwa urefu wa mita 1.2 toka sakafuni na kiringe cha kunadi.
ii) Vifaa vya kulisha na kunywea maji,
iii) Tanuru/shimo la kuteketeza/kuzika mizoga na taka nyingine,
iv) Ofisi, nyumba ya mlinzi na vyoo vinavyokidhi mahitaji,

v) sehemu ya kuchinjia kwa dharura (emergency slaughter slab)
vi) Jiko la kuchemshia maji
vii) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada.

### 3.1.3 Minada ya Upili na Mipakani

Minada ya upili na mipakani itaanzishwa kwa kibali cha Waziri mwenye dhamana ya maendeleo ya mifugo, itasimamiwa na itaendeshwa na wizara hiyo. Minada ya upili na ya mipakani itatangazwa kwenye Gazeti la Serikali kabla ya kuanza kutumika. Vile vile minada ya awali inaweza kupandishwa hadhi na waziri mwenye dhamana ya mifugo kuwa minada ya upili au ya mipakani endapo itafikia vigezo ambavyo ni:-

i) Kuwa kwenye eneo ambalo njia za mifugo zinakutana
ii) Kuwa karibu na miji mikubwa yenye walaji wengi au karibu na mpaka wa nchi
iii) Kuwa na biashara ya mifugo ya zaidi ya ng'ombe **500** kila siku au zaidi ya ng'ombe **700** kwa wiki.

#### 3.1.3.1 Mchoro na ujenzi wa minada ya upili na mipakani

Minada ya upili na mipakani ijengwe kwa kufuata michoro iliyohakikiwa ili kuweka viwango vya ubora vilivyokubalika na kuwa na mfumo mmoja wa ujenzi wa minada hapa nchini. Ili kuwa na mfumo huo utaratibu ufuatao uzingatiwe:-

(a) Mchoro wa mnada wa mifugo utaandaliwa na Wizara yenye dhamana ya mifugo.
(b) Ujenzi wa mnada uzingatie Sheria ya Ununuzi ya Umma ya Mwaka 2004 na kanuni zake za mwaka 2005,

#### 3.1.3.2 Mchoro wa mnada wa ng'ombe, mbuzi na kondoo

i) Sehemu ya kushusha na kupakia mifugo.
ii) Mazizi ya mifugo inayouzwa, iliyonunuliwa na mifugo iliyotengwa kwa sababu mbalimbali,
iii) Mizani, kibanio, kiringe cha kunadi mifugo na majukwaa ya wauzaji na wanunuzi,
iv) Mabirika ya maji na eneo la malisho.
v) Eneo maalum la kupumzishia mifugo kwa ajili ya kuzuia kupungua kwa uzito (recover weight loss) unaotokana na usafirishaji wa mifugo kwa muda mrefu na ukaguzi wa afya ya mifugo kabla ya kuchinjwa au kusafirishwa nje ya nchi.
vi) Josho au kinyunyizio cha dawa ya kuua kupe.
vii) Tanuru/shimo la kuteketeza/kuzika mizoga na taka nyingine
viii) Ofisi ya mnada, kituo kidogo cha polisi wa kuzuia wizi wa mifugo, nyumba za wafanyakazi na waswagaji na vyoo vinavyokidhi mahitaji,
ix) sehemu ya kuchinjia kwa dharura (emergency slaughter slab)
x) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada.

#### 3.1.3.3 Mchoro wa mnada wa nguruwe

i) Sehemu ya kupakia na kushusha nguruwe,
ii) Mazizi yenye paa kwa ajili ya nguruwe wanaouzwa, walionunuliwa na waliotengwa kwa sababu mbalimbali,
iii) Mizani, kibanio, kiringe cha kunadi nguruwe na majukwaa ya wanunuzi na wauzaji,
iv) Mabirika ya maji na eneo la kulishia ndani ya mazizi,
v) Tanuru/shimo la kuteketeza/zika mizoga na taka nyingine,
vi) Ofisi ya mnada, kituo kidogo cha polisi wa kuzuia wizi wa mifugo, nyumba za wafanyakazi na wasafirishaji, maji na vyoo vinavyokidhi mahitaji,
vii) Sehemu ya kuchinjia kwa dharura (emergency slaughter slab),
viii) Jiko la kuchemshia maji,
ix) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada.

#### 3.1.3.4 Mcharo wa mnada wa kuku

i) Mabanda kwa ajili ya kuku wanaouzwa, walionunuliwa, waliotengwa kwa sababu mbalimbali, yaliyo simikwa urefu wa mita 1.2 toka sakafuni na kiringe cha kunadi.
ii) Vifaa vya chakula na maji,
iii) Tanuru/shimo la kuteketeza/kuzika mizoga na taka nyingine,
iv) Ofisi ya mnada, kituo kidogo cha polisi wa kuzuia wizi wa mifugo, nyumba za wafanyakazi na wasafirishaji na vyoo vinavyokidhi mahitaji,
v) Sehemu ya kuchinjia kwa dharura,
vi) Jiko la kuchemshia maji, na
vii) Uzio wa kuzunguka eneo la mnada.

### 3.1.4 Mizani

Sheria ya Vipimo na Mizani Na. 20 ya mwaka 1982, kifungu Na. 11 kinaelekeza matumizi ya mizani katika biashara na kifungu Na. 26 kinaelekeza kuuza bidhaa kwa kutumia vipimo na mizani. Sheria hii inataka biashara ya mifugo ifanyike kwa kutumia mizani na bila kufanya hivyo ni kuvunja sheria. Inaelezwa kuwa kuna aina mbili za mizani ya kupima ng'ombe ambazo ni za Electronic display ambazo zina mahitaji sawa ya viwango vya chini vya ubora vya mzani. Mizani hizi zinatofautiana uwezo wa kupima ng'ombe, aina ya kwanza ina uwezo wa kupima uzito usiozidi **tani 10** kwa mara moja (takribani ng'ombe 20) na aina ya pili ina uwezo wa kupima uzito usiozidi **tani 5** kwa mara moja (takribani ng'ombe 10).

Vile vile kuna aina mbili za mizani za kupimia Kondoo na Mbuzi ambazo pia zinatofautiana kwa uwezo wa kupima uzito ambao ni uzito usiozidi **tani 1** kwa mara moja (takribani mbuzi 40) au uzito usiozidi **tani 0.5** kwa mara moja (takribani mbuzi 20). Viwango vya ubora vinavyohitajika kwa mizani zote hapo juu ni:-

i) Itengenezwe na chuma kizito kisichoshika kutu na kiwe na eneo pana (platform) la mita za mraba 25 kwa ajili ya kusimamia mifugo

ii) Kizimba cha chuma kizito chenye kuta imara na milango (gates) inayofungwa ili kudhibiti mifugo
iii) Iwe na eneo kubwa la kusomea vipimo vya uzito (**inch 3.0 urefu**) electronic system - LCD display na iwe na kifungo cha kuzungusha kuchagua ili kuwa rahisi kutumia
iv) Iwe na sehemu tatu za kunakili uzito kwa uharaka na urahisi wa kupima.
v) Iwe na uwezo wa kuhimili vishindo na isiyoruhusu maji kuingia.
vi) Ijengewe baterii inayoweza kuongezewa umeme yenye alama ya kuonyesha mwenendo wa umeme (low-voltage shutdown).
vii) Iwe na uwezo wa kusoma uzito wa mifugo bila kujali kama mifugo inatembea tembea.
viii) Ifanye kazi katika umeme wa AC 22-240V , 50HZ
ix) Iwe na uwezo wa kutunza kumbukumbu zisizopungua **16,000** na taarifa za kila mfugo au kundi au batch au majina
x) Iwe na sehemu za kuunganisha kuprinti zisizopungua 2.

Vigezo vingine vinavyohitajika kwenye mizani ni pamoja na

i) Iwe na uwezo wa kutunza uzito wa mifugo iliyopimwa kwa dakika chache zaidi baada ya mifugo kutoka kwenye mizani. Vile vile iwe na uwezo wa kutoa uzito usio wa mifugo au uzito wa mhudumu ili kupunguza uwezekano wa kuwa na makosa ya kimahesabu.
ii) Kigezo kingine kinachohitajika kwa baadhi ya mizani za electronic ni uwezo wa kutumiwa kwenye maeneo ya baridi na ya joto.
iii) Muunganisho wa RS232 mara nyingi unahitajika kwenye mizani za mifugo minadani ambazo zinauwezo wa kuhamisha takwimu moja kwa moja kwenda kwenye printer, komputa au kifaa cha kusoma alama za masikioni (ear tag reader). Baadhi ya mizani hizi zina uwezo wa kupanga takwimu.
iv) Baadhi ya mizani za electronic zina nafasi ya kuzidisha uzito kwa asilimia 100 au zaidi. Hii inamaanisha kwamba uwezo wa ziada unaweza kuongezeka bila kuharibu mizani, jambo ambalo linaweza kutokea wakati mwingine.



**Picha 1: Mzani wa kupimia uzito wa Mifugo na kiringe cha kunadia**

**Kumbuka:** Zipo aina chache za mizani hizi ambazo zina uzito mdogo wa kiasi cha kilo 1000 na zinaweza kuwekwa shambani kwa ajili ya kupima mifugo shambani. Mizani hizi zina hamishika na zina miguu inayoweza kurekebishika ili kupunguza tatizo la kutolingana kwa sakafu. Baadhi yake zinaletwa na indicator ya pembeni lakini indicator za wima zinakuwepo pia.

## 3.2 Usimamizi na Uendeshaji wa Minada

Ufanisi katika uendeshaji wa minada ya mifugo hutegemea usimamizi mzuri, vitendea kazi vya kutosha na miundombinu inayokidhi mahitaji ya mnada. Sheria ya Nyama Na. 10 ya mwaka 2006, Kanuni ya Uendeshaji wa Masoko ya Mifugo kifungu Na. 10 (1 na 2) inaelekeza watumishi wanaohitajika katika mnada. Mnada uwe na watumishi wa kutosha na wenye sifa, maadili ya kazi, mipango mizuri na utunzaji wa kumbukumbu.

### 3.2.1 Majukumu ya wafanyakazi katika mnada

Katika mnada kutakuwa na wafanyakazi wafuatao mkuu/msimamizi wa minada wa wilaya, afisa mkaguzi wa afya ya mifugo, mhasibu, dalali, mpanga madaraja ya mifugo na mkuu wa usalama wa raia mnadani ambao majukumu yao ni kama ifuatavyo:-

#### 3.2.1.1 Mkuu wa mnada/ Msimamizi wa minada wa wilaya

Mkuu wa Mnada (Market Master) ndiye msimamizi mkuu wa shughuli zote za utawala na biashara ya mifugo katika mnada, ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kusimamia utendaji kazi wa wafanyakazi wote katika mnada,
(b) Kuwajibika kulinda na kutunza mali za mnada kwa niaba ya mamlaka inayosimamia mnada huo ikiwa ni pamoja na kulinda mipaka ya eneo la mnada na eneo la kupumzikia mifugo,
(c) Kusimamia biashara ya mifugo ikiwa ni pamoja na kuhakiki leseni za wafanyabiashara na ukusanyaji wa maduhuli,
(d) Kupokea mifugo inayoingia mnadani na kutoa idhini ya kutoa mifugo iliyouzwa baada ya kuridhika kuwa taratibu zote za mnada zimefuatwa,
(e) Kukusanya, kutunza, kuchambua takwimu na kutoa taarifa za mwenendo wa biashara ya mifugo, ikiwa ni pamoja na kuandika bei za mifugo kwenye ubao wa mnada,
(f) Kuandaa taarifa za wiki, mwezi na mwaka za utekelezaji wa shughuli za mnada na kuwasilisha kwa mamlaka husika kama vile Serikali za Mitaa, Wizara zenye dhamana ya mifugo, ya biashara, vyama vya wafugaji na vya wafanyabiashara,
(g) Kupanga ratiba ya siku za mnada kwa mwaka na kuwasilisha kwa wadau ikiwa ni pamoja na wizara yenye dhamana ya mifugo, na
(h) Mkuu wa mnada atawajibika kwa mamlaka iliyomteua.

#### 3.2.1.2 Afisa Mkaguzi wa Afya ya Mifugo

Afisa mkaguzi wa afya ya mifugo atatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Na. 17 ya mwaka 2003 ya Magonjwa ya Wanyama na Kanuni zake ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kupokea mifugo wanaoingia mnadani na kuhakiki uhalali wa vibali vilivyotumika kusafirishia mifugo,
(b) Kukagua na kuchunguza afya za mifugo yote inayoingia mnadani kabla ya kuanza kuuzwa,
(c) Kukagua afya ya mifugo yote iliyonunuliwa na kutoa vibali vya kusafirishia.
(d) Kutunza kumbukumbu za vibali, idadi ya mifugo inayoingia na kutoka mnadani,
(e) Atawajibika kuandaa na kutoa taarifa za magonjwa ya mifugo,
(f) Atawajibika kwa mkuu wa mnada, na
(g) Kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mkuu wa Mnada.

#### 3.2.1.3 Mhasibu

Mhasibu atamsaidia mkuu wa mnada katika kuhakikisha kuwa taratibu zote za ukusanyaji wa maduhuli ya serikali zinafuatwa ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kukusanya ushuru wa soko na wa vibali vya kusafirishia mifugo na kuwasilisha sehemu husika,
(b) Kuweka na kuwasilisha taarifa za maduhuli ya Serikali kwa mamlaka husika,
(c) Kumshauri mkuu wa mnada njia mwafaka za kuongeza makusanyo,
(d) Atawajibika kwa Mkuu wa Mnada, na
(e) Kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mkuu wa Mnada.

#### 3.2.1.4 Dalali

Dalali kwa kushirikiana na mkuu wa mnada atawajibika kuhakikisha kuwa ratiba ya biashara ya mnada inafuatwa kama ilivyopangwa ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kuanzisha mnada kwa kutoa ishara (kupiga filimbi, kengele, n.k.)
(b) Kunadi kwa haki mifugo iliyoletwa mnadani,
(c) Kuhakikisha biashara ya mifugo inakamilishwa kwa kubadilishana vibali kati ya mnunuzi na muuzaji,
(d) Kutoa taarifa za mwenendo wa bei za mifugo,
(e) Kufunga mnada kwa kutoa ishara (kupiga filimbi, kengele, n.k.).
(f) Atawajibika kwa Mkuu wa Mnada, na
(g) Kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mkuu wa Mnada.

#### 3.2.1.5 Mpanga madaraja ya mifugo

Mpanga madaraja ya mifugo atatakiwa kuhakikisha biashara ya mifugo katika mnada inafanywa kwa kuzingatia madaraja, ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kupima uzito mifugo yote iliyoletwa mnadani na kuipanga katika madaraja ya ubora,

(b) Kwa kushirikiana na Mkuu wa Mnada kuzuia mifugo yote ya daraja la chini (Daraja la tatu na la nne) na wenye mimba wasiuzwe kwa nia ya kuchinja,
(c) Kukusanya, kutunza, kuchambua na kutoa taarifa za madaraja ya mifugo,
(d) Atawajibika kwa mkuu wa mnada, na
(e) Kazi nyingine kama atakavyoelekezwa na Mkuu wa Mnada.

#### 3.2.1.6 Mkuu wa usalama wa raia na mali mnadani

Mkuu wa usalama wa raia na mali mnadani atawajibika kuweka mazingira ya usalama na amani katika eneo la mnada ili kuwezesha biashara ya mifugo kufanyika kwa ufanisi ikiwa ni pamoja na:-

(a) Kushirikiana na Mkuu wa Mnada kufanya utambuzi wa mifugo iliyoletwa mnadani na kuchunguza wanakotoka kwa sababu za kiusalama,
(b) Kuhakikisha usalama wa watu na mali zao katika eneo la mnada,
(c) Kuhakikisha usalama wa maduhuli ya serikali,
(d) Kusaidia kuzuia uharibifu wa miundombinu ya mnada ikiwemo mipaka ya eneo la mnada, na
(e) Atawajibika kwa Mkuu wa Mnada katika shughuli za biashara ya mifugo.

## 3.3 Ratiba ya mnada

Ratiba ya mnada iandaliwe ili kupunguza mwingiliano wa shughuli za minada na kuwasaidia wafugaji na wafanyabiashara kujua siku za minada kama ifuatavyo:-

(a) Mkuu wa Mnada wa upili/mpakani au Msimamizi wa Minada wa wilaya, kwa kushirikiana na wadau husika (kama vile kikundi cha wafanyabiashara ya mifugo) kuandaa ratiba ya shughuli za mnada,
(b) Mkuu wa Mnada wa upili/mpakani au Msimamizi wa Minada wa wilaya awasiliane na ofisi zinazohusika na masoko ya mifugo katika maeneo ya karibu ili kuepuka muingiliano wa ratiba ya siku na shughuli za minada,
(c) Mkuu wa Mnada aufahamishe umma kuhusu ratiba ya shughuli za mnada kupitia vyombo vya habari na mbao za matangazo,
(d) Shughuli za mnada zitaanza saa 3:00 asubuhi na kufungwa saa 9:00 alasiri kwa siku za mnada, na
(e) Ratiba za minada za wilaya zote ziwasilishwe mkoani kwa ajili ya kuandaa ratiba ya minada ya mikoa na hatimaye kuwasilisha wizarani kwa ajili ya kuandaa ratiba ya minada kitaifa.

## 3.4 Usafi, ukarafati, ukarabati na ulinzi wa minada

### 3.4.1 Usafi

Mnada ni eneo ambalo huwa na mkusanyiko mkubwa wa watu, hivyo kuna umuhimu wa kuzingatia kanuni za afya. Maeneo ya kuuzia mifugo (mazizi) na maeneo mengine ya kutolea huduma mnadani yawe safi kwa kuzingatia yafuatayo:-

(a) Mkuu wa Mnada atasimamia na kuhakikisha eneo la soko linakuwa safi na kukidhi viwango vya afya,

(b) Mazizi ya minada yawe na sakafu madhubuti ambayo itarahisisha kufanyia usafi. Sakafu inatakiwa kuwa na mwinuko (angalau 2%) ambao hauruhusu kutuama maji.
(c) Samadi inayotokana na mifugo inatakiwa kuondolewa kutoka mazizini mara kwa mara na kurundikwa kwenye eneo lililotengwa kwa ajili ya matumizi mbalimbali (Kilimo na uzalishaji wa nishati ya gesi),
(d) Mabanda/migahawa ya kutolea huduma ya chakula katika eneo la mnada yawe kwa mpango maalum unaoruhusu usafi kufanyika kwa urahisi,
(e) Kuwe na huduma ya maji salama na ya kutosha kwa ajili ya matumizi ya binadamu na mifugo,
(f) Kuwe na vifaa maalum vya kutosha kukusanya taka ngumu,
(g) Kuwe na mifereji inayotiririsha majitaka kwenda kwenye mkondo au shimo, na
(h) Kuwe na vyoo vya kutosha kukidhi mahitaji.

### 3.4.2 Ukarafati na ukarabati wa minada

Ujenzi wa miundombinu ya minada ni wa gharama kubwa na hivyo miundombinu inahitaji kutunzwa kwa kufanya ukarafati wa mara kwa mara. Asilimia 15 ya ushuru wa soko unaobakia katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ingizwe kwenye Mfuko wa Maendeleo ya Mifugo (LDF) wa Mamlaka husika ambao utatumika kuendeleza na kuboresha huduma za mifugo ikiwemo ukarabati wa miundombinu na uendelezaji wa masoko ya mifugo ndani ya Mamlaka husika. Aidha, wizara yenye dhamana ya mifugo itaendelea kutenga bajeti kwa ajili ya ukarabati wa minada ya upili na ile ya mipakani.

### 3.4.3 Ulinzi wa minada

Minada ina miundombinu yenye gharama kubwa. Ili kuzuia uharibifu wa miundombinu hiyo kwa njia ya wizi au uharibifu wa makusudi hatua zifuatazo zichukuliwe;
(a) Mkuu wa mnada/msimamizi wa mnada wa wilaya ahakikishe usalama wa mipaka na miundombinu ya mnada,
(b) Mkuu wa mnada/msimamizi wa mnada wa wilaya achukue hatua za haraka endapo utatokea uvamizi wa mipaka au uharibifu wa miundombinu, na
(c) Mkuu wa mnada/msimamizi wa mnada wa wilaya ahakikishe ulinzi wa mifugo wanaosubiri kusafirishwa na wale wanaosubiria siku ya soko.

## 4.0 Hitimisho

Biashara ya mifugo imekuwa ikifanyika hapa Tanzania kwa kipindi kirefu kama muhimili mkubwa wa sekta ya mifugo katika kunufaisha mfugaji na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo biashara hii imekuwa ikifanyika bila utaratibu mzuri na kusababisha mchango mdogo wa sekta ya mifugo katika pato la Taifa. Hii ni kwa sababu taratibu, uangalizi na uwekaji wa kumbukumbu katika Biashara ya mifugo ulikuwa dhaifu.

Mwongozo huu wa masoko ya mifugo umeandaliwa ili kuweka taratibu katika uangalizi na uwekaji wa kumbukumbu ili kuboresha biashara ya Mifugo. Vile vile kutoa mwongozo wa namna ya kuanzisha, kuendesha na kusimamia miundombinu ya masoko na shughuli za minada ili kuleta tija na uendelevu.